AFRICAN UNION

الاتحاد الأفريقي

UMOJA WA AFRIKA

UNION AFRICAINE

UNIÃO AFRICANA

UNIÓN AFRICANA

Addis Ababa, Ethiopia S.L.P 3243 Simu: +251 115 517 700 Nukushi : +251 115 517 844
Tuvuti: www.au.int

BARAZA KUU
Mkuatano wa Arobaini na nne wa Kawaida
Tarehe 15 Januari - 15 Februari 2024
Addis Ababa, ETHIOPIA

EX.CL/1501(XLIV)
Annex
Matini chanzi: Kiingereza

RIPOTI YA MAENDELEO YA UTEKELEZAJI WA UAMUZI WA MKUTANO MKUU (Assembly/AU/Dec.847(XXXVI)) JUU YA KUWEKA MSIMAMO MMOJA WA VUGUVUGU LA KUPIGANIA HAKI NA MALIPO YA FIDIA KWA WAAFRIKA.

RIPOTI YA MAENDELEO YA UTEKELEZAJI WA UAMUZI WA MKUTANO MKUU (Assembly/AU/Dec.847(XXXVI)) JUU YA KUWEKA MSIMAMO MMOJA WA VUGUVUGU LA KUPIGANIA HAKI NA MALIPO YA FIDIA KWA WAAFRIKA.

1. Itakumbukwa kuwa Februari 2023, Mkutano wa 36 wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika ulipitisha Uamuzi, Rej., Assembly/AU/Dec.847(XXXVI), juu ya Kuweka Msimamo mmoja wa Kuendeleza Vuguvugu la kupigania Haki na Malipo ya Fidia kwa Waafrika. Katika Uamuzi huo, Mkutano Mkuu, pamoja na mambo mengine, uliitaka Kamisheni kuwasilisha ripoti ya maendeleo ya utekelezaji wake kwenye Mkutano wake wa 37 wa Kawaida.

2. Kwa hiyo, Kamisheni itawasilisha ripoti hii katika kutimiza wajibu wake wa kuripoti kwenye Mkutano Mkuu kabla ya tarehe ya mwisho ya Februari 2024 kama ilivyoainishwa katika Uamuzi uliotajwa hapo juu.

3. Itakumbukwa zaidi kwamba Uamuzi wa Mkutano Mkuu uliidhinisha pendekezo lililotolewa na Serikali ya Ghana la kuandaa pamoja na wadau husika na kuandaa Kongamano la Kimataifa mwaka 2023 kuelekea “Kuweka Msimamo mmoja wa Kuendeleza Vuguvugu la kudai Haki na Malipo ya Fidia kwa Waafrika”. Kwa maana hiyo, Kamisheni iliombwa kushirikiana na Serikali ya Ghana katika maandalizi ya Mkutano huo.

4. Kwa kuzingatia yaliyotajwa hapo juu, Kamati ya Uratibu ya dharula, inayojumuisha Ubalozi wa Kudumu wa Ghana kwenye Umoja wa Afrika na Tume iliundwa. Kamati hii iliitisha mfululizo wa vikao ili kuwezesha Mkutano huo. Shughuli kadhaa pia zilifanyika wakati wa maandalizi. Miongoni mwa shughuli hizi ilikuwa ni ziara ya mafunzo kuhusu Malipo ya fidia na Haki ya watu wenye Rangi mbalimbali iliyoandaliwa na Serikali ya Barbados, kuanzia tarehe 24 hadi 28 Julai, 2023, na kuhudhuriwa na wawakilishi wa Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu (PRC), yaani, MHE Youssouf Mandoha Assoumani, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Wawakilishi (PRC) na Mwakilishi wa Kudumu wa Comoro kwenye AU, na Mwakilishi wa Kudumu wa Ghana kwenye umoja wa Afrika, MHE. Amma Twum-Amoah. Ilitimiza madhumuni ya kuweka msingi wa uhusiano ulioimarishwa kati ya Afrika na diaspora yake, mshirika wa lazima katika jitihada zetu za pamoja za kufuatilia madai ya fidia katika ngazi ya kimataifa.

5. Mkutano wenyewe ulikusudiwa kujikita kwenye mipango ya zamani, iliyofanywa kuhusiana na madai ya fidia, na ambapo bara la Afrika lilihusika. Hizi ni pamoja na Kongamano la kimajumui la iliyokuwa OAU kuhusu malipo ya fidia lililofanyika Abuja, (1993); Mkutano wa Dunia wa Kupinga Ubaguzi wa Rangi, Ubaguzi kwa misingi ya asili ya mtu, chuki dhidi ya wageni na Kutovumiliana uliofanyika chini ya usimamizi wa Umoja wa Mataifa mjini Durban (2001); na Kongamano la Accra kuhusu Kupigania Haki: Malipo ya fidia na Usuluhishi baina ya jamii ya watu weupe na weusi (2022). Kufanyika kwa Kongamano hilo kuliashiria hatua kubwa ya kusonga mbele katika juhudi zetu za pamoja kama bara la Afrika la kuimarisha harakati za kudai malipo ya fidia duniani kote ambazo zilikuwa zikishika kasi.

6. Mkutano wa Accra kuhusu Malipo ya fidia (ARC) kwa hiyo ulifanyika Accra, Ghana kuanzia tarehe 14 hadi 17 Novemba, 2023.

7. Mkutano huo ulifunguliwa na MHE. Nana Addo Dankwa Akufo-Addo, Rais wa Jamhuri ya Ghana, ambaye alitoa Hotuba Kuu. Aliyehudhuria pia, alikuwepo Mheshimiwa Azali Assoumani, Rais wa Muungano wa Comoro, na Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika (AU). Mawaziri Wakuu wa Burundi, Barbados na Togo, na Mawaziri wa Nchi Wanachama wa AU, pamoja na Katibu Mkuu wa CARICOM, pamoja na watu wengine wakuu wa diaspora, pia walitoa hotuba muhimu.

8. Makamu Mwenyekiti wa Kamisheni, Dkt. Monique Nsanzabaganwa, aliyemwakilisha Mwenyekiti wa Kamisheni, MHE. Moussa Faki, pia alisoma ripoti kwa niaba yake. Miongoni mwa waliohudhuria pia walikuwepo wataalamu wa sheria, watunga sera, wasomi na wadau kutoka Umoja wa Afrika na wanadiaspora wa Afrika.

9. Wakati wote wa mijadala ya Mkutano huo, kimsingi ilikubaliwa kwamba kulikuwa na uhalali wa kimaadili na kisheria ya madai ya fidia kuhusiana na dhulma za kihistoria na uhalifu wa kudhuru uliofanywa dhidi ya Waafrika na Watu wa asili ya Kiafrika. Hizi ni pamoja na utumwa uliovuka bahari ya Atlantiki, ukoloni, mauaji ya halaiki na ubaguzi wa rangi; na ilisisitizwa kwamba kufuatilia madai ya fidia kungefungua njia ya kuendeleza vuguvugu la kudai haki ya malipo ya fidia kwa Waafrika na watu wote wenye asili ya Kiafrika.

10. Ilikubaliwa zaidi kwamba kulikuwa na haja ya kushughulikia pia ukosefu wa usawa unaodhihirisha mifumo ya sasa ya ukoloni mamboleo wa kimataifa katika nyanja za kiuchumi na kisiasa.

11. Kwa kuona mbali, ilitiliwa mkazo kwamba kulikuwa na haja ya kuimarisha harakati za kudai malipo ya fidia kwa kuanzisha taasisi na taratibu ambazo zingeipa muundo, kukuza kasi yake na kuhakikisha inakuwa endelevu.

12. Kwa hiyo, mapendekezo yafuatayo (kama yalivyofafanuliwa katika Azimio la Accra lililopitishwa mwishoni mwa Mkutano na kuambatanishwa kama Kiambatisho cha Ripoti ya Maendeleo ya sasa) yalitolewa; na Kamisheni itawasilisha mapendekezo haya kama yanafaa kuzingatiwa:

i. Kamati ya Wataalamu wa Malipo ya fidia: Kunapaswa kuwa na uthibitisho mpya wa agizo lililomo kwenye Uamuzi wa Mkutano Mkuu (Assembly/AU/Dec.847(XXXVI)) kuhusu kuundwa kwa Kamati ya Wataalamu wa Malipo ya fidia na Kamisheni, kwa kushauriana na Nchi Wanachama, ECOSOCC na vyombo vingine vya AU pamoja na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda. Hii itakuwa kwa madhumuni ya kuandaa Sera moja ya Kiafrika ya Madai ya fidia na kuijumuisha ndani yake;

ii. Ofisi ya Mjumbe Maalum wa AU kuhusu Malipo ya fidia: Ili kuimarisha kazi ya Kamati ya Wataalamu, Ofisi ya Mjumbe Maalum wa AU wa Malipo ya fidia inapaswa kuundwa

kwa mujibu wa taratibu zinazostahili za Kamisheni ya AU, na kwa kushauriana na Baraza Kuu , kwa kuzingatia hasa mamlaka yake.
iii. Utafiti wa chaguzi za kisheria na kimahakama kwa ajili ya kudai fidia: Kunapaswa kuungwa na AU yote kwa hatua zinazochukuliwa ndani na nje ya bara na nchi wanachama na waathiriwa na vizazi vyao kuhusiana na uhalifu wa kihistoria, na pia kwa ajili ya kesi za baadaye za madai ya fidia. Ikumbukwe kwamba vyombo husika vya AU, ikiwa ni pamoja na Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu, Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu, Tume ya Umoja wa Afrika ya Sheria za Kimataifa siku za nyuma, vilifanyia kazi suala la masuala ya kisheria ya malipo ya fidia, ushirikiano kati yao pamoja na vyombo vingine vya AU unapaswa kuhimizwa, kwa kuzingatia namna ambavyo sheria za kimataifa zinavyoingiliana na au, kuunga mkono jitihada za madai ya fidia. Sambamba na hilo, kuwe na ushirikiano kati ya vyombo husika vya AU kwa upande mmoja, na vyombo wenzao katika CARICOM, Amerika ya Kusini na maeneo mengine ya diaspora, pamoja na Umoja wa Mataifa na mashirika mengine husika ya kimataifa.

iv. Mashirika na Taasisi za AU kushiriki zaidi na kikamilifu: Kwa ujumla, vyombo na taasisi za AU zinapaswa kushiriki zaidi na kikamilifu, kama vile Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu, Mahakama ya Afrika, AUCIL, ECOSOCC, PAP, ACERWC, Bodi ya Ushauri ya AU Dhidi ya Ufisadi, pamoja na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda katika kampeni ya kudai fidia. Hili linapaswa kutekelezwa kwa uratibu wa karibu na Kamisheni ya Umoja wa Afrika, ili kuchukua hatua madhubuti, kukuza na kudumisha uhusiano kati yao.

v. Timu ya Wataalam wa Sheria: Timu ya wanasheria ambayo itafanya kazi kwa uratibu wa karibu na Kamisheni ya Umoja wa Afrika, inapaswa kuundwa ili kusaidia Kamati ya Wataalamu wa AU na Mjumbe Maalum wa AU. Timu hii ya wanasheria itatoa ushauri wa kisheria kuhusu suala la fidia ikijumuisha, mbinu bora za kisheria kuhusu sheria na madai yanayoathiri ajenda ya malipo ya fidia. Timu ya wanasheria msaada wa kitaalam na ushauri, kutokana na tafiti za kimataifa, ili kuiboresha sera.

vi. Kutambua juhudi za Mashirika ya Kiraia ya Kiafrika kuhusiana na malipo ya fidia: Kwa nia ya kuendeleza kazi iliyofanywa na Kamisheni ya AU na ECOSOCC, kupitia taasisi za serikali na zisizo za kiserikali zenye raia wa Afrika, kupitia watendaji wa mashirika ya kiraia, ikiwa ni pamoja na jumuiya ya diaspora ya Afrika. Hii itawezesha mijadala ya kila siku kupata taarifa sahihi kuhusu madai ya fidia na haki ya malipo ya fidia.

vii. Uundaji wa Mfumo wa Ushirikiano wa Kuvuka Bara: Mfumo wa ushirikiano wa kuvuka bara kati ya AU, CARICOM, na wanadiaspora wa Afrika katika bara la Amerika ya Kusini, Amerika ya Kaskazini, Ulaya, Uingereza na maeneo mengine yote duniani, unapaswa kuanzishwa, kwa nia ya kukuza ushirikiano na mshikamano ndani ya Nchi za Kusini (Global South). Hii itatokana na kutambua kwamba fidia ni nguzo muhimu kwa maendeleo endelevu.

viii. Kuongezeka kwa jukumu la Umoja wa Mataifa: Katika muktadha wa Umoja wa Mataifa kwa mapana zaidi, Jukwaa la Kudumu la Umoja wa Mataifa la Watu Wenye Asili ya Afrika, linaweza kufikiria kuitisha, kwa uratibu wa karibu na Kamisheni ya Umoja wa

Afrika, Mkutano wa Kimataifa, unaohusisha madola ya zamani ya kikoloni, kuhusu. suala la fidia, pamoja na kuongeza Muongo kwa Watu wenye asili ya Kiafrika.

ix. Urejeshwaji, Urejeshaji na Ulindaji wa Mali za Kitamaduni za Kiafrika: Kwa kuzingatia masharti husika ya Ajenda 2063 ya Umoja wa Afrika, ambayo yanataka kurejeshwa kikamilifu na kulindwa kwa utamaduni ulioporwa wa Afrika, urithi na vitu vya kale, Msimamo thabiti wa Afrika wa Pamoja juu ya Urejeshaji wa mali. Mali ya Utamaduni na Urithi inapaswa kuendelezwa. Zaidi ya hayo, Mfumo wa Utekelezaji wa Majadiliano ya Kurejesha/Urejeshaji wa mali ya kitamaduni iliyosafirishwa kinyume cha sheria kutoka Barani kwa mujibu wa Mashauriano ya Bara juu ya Urejeshaji wa Mali za Kitamaduni na Turathi yaliyofanyika kuanzia tarehe 30 Novemba hadi 2 Desemba 2021 inapaswa kutolewa.

x. Mfuko wa Malipo ya fidia Duniani: Mfuko wa Kimataifa wa Fidia ili kuendeleza kampeni ya kudai fidia barani Afrika unapaswa kuanzishwa kwa ushirikiano wa karibu na Umoja wa Afrika.

xi. Kuweka msimamo mmoja wa Kukabiliana na Ukosefu wa Usanifu wa Kifedha wa Kimataifa wa Ukoloni Mamboleo: Kupitia mageuzi ya mifumo na miundo ya usanifu wa kifedha wa ukoloni mamboleo, kama ilivyopendekezwa katika mataifa mengine ya kimataifa kwa Wakuu wa Nchi za Kiafrika ikiwa ni pamoja na wale wa Kenya, Afrika Kusini na Ghana, zinapaswa kuanzishwa. Hii itakuwa kwa nia ya kufikia miundombinu mipya ya kifedha ya kimataifa ikiwa ni pamoja na taasisi za Bretton Woods, ambayo ni ya urekebishaji kwa asili na yenye usawa kiuchumi katika wigo na kiutendaji. Katika hali hiyo hiyo, taratibu za hasara na uharibifu, mabadiliko ya hali ya hewa, msamaha wa madeni, kuzuia mzunguko wa fedha haramu zinapaswa kuanzishwa.

xii. Kuungana na kuwa msitari wa mbele katika kukabiliana na mfumo wa kibepari wa kimataifa wa fedha na Ukoloni Mamboleo: Msimamo mmoja unapaswa pia kuwekwa ili kukabiliana na ukosefu wa usawa uliopo katika mfumo wa kisiasa wa kimataifa, kwa kuzingatia hasa muundo na kanuni za Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kama inavyopiginiwa mara kwa mara na AU.

xiii. Kongamano la Kila Mwaka la Kimataifa la Fidia: Kwa ushirikiano na Kamisheni ya AU, Nchi nyingine Wanachama wa AU zinapaswa kuhimizwa kujitolea kuwa mwenyeji wa Mkutano huo unaofanyika kila mwaka, pamoja na taratibu nyingine muhimu za mazungumzo yanayohusiana na vipengele maalum vya malipo ya fidia, ili kuendeleza harakati hiyo.

xiv. Kaulimbiu ya Mwaka 2025: Kaulimbiu ya mwaka 2025 inapaswa kuwa “Haki kwa Afrika kwa njia ya Malipo ya fidia”.

AFRICAN UNION UNION AFRICAINE

African Union Common Repository **http://archives.au.int**

Organs Council of Ministers & Executive Council Collection

2024-01-15

Progress report on the Implementation of the Assembly Decision (Assembly/Au/Dec.847(Xxxvi)) on building a United Front to Advance the Cause of Justice and the Payment of Reparations to Africans

African Union

https://archives.au.int/handle/123456789/10541

Downloaded from African Union Common Repository